JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

"Kilimani" Iringa Road,
S.L.P. 1175,
41101 DODOMA,
Barua Pepe: rbcdodoma@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

DODOMA – APRILI 10, 2022

WAKAZI WA MKOA WA DODOMA WAKUMBUSHWA WAJIBU WA KUSHIRIKI KUZUIA VITENDO VYA RUSHWA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika robo ya Januari hadi Machi, 2022 ambapo mkazo uliwekwa katika elimu ya kuhamasisha wananchi ili washiriki kikamilifu kuzuia rushwa kwakuwa rushwa huzorotesha maendeleo ya jamii. Ukilinganisha kazi za uelimishaji zilizofanyika katika robo hii mwaka jana, kuna ongezeko la asilimia 115 la kazi za uelimishaji kwa robo ya mwaka huu. **Kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:**

Uelimishaji Umma:

Na	KAZI	UFAFANUZI
1	Elimu ya kubadili mtizamo wa makundi ya wananchi ili watambue wajibu wao wa kushiriki kivitendo kuzuia vitendo vya rushwa kabla ya kutokea	Elimu hii ilitolewa kwa kulenga rika la vijana kupitia Klabu za Wapinga Rushwa na kuelimisha Wanachama wa SKAUTI kupitia mkakati wa ushirikiano kati ya TAKUKURU na SKAUTI (TAKUSKA).
2	Kampeni maalum ya kuwafuata wananchi kwenye mikusanyiko na kuwaelimisha kupitia vipaza sauti, huku wakiendelea na shughuli zao, **ULIPO TWAJA.**	Elimu hii ililenga wananchi wa rika la miaka 15 hadi 64, ambao zaidi ndio huwepo kwenye mikusanyiko hiyo. • Kampeni ya ULIPO TWAJA ilifanikiwa kuelimisha mikusanyiko 127 ambapo takribani wananchi 120,077, ambao ni asilimia 86 ya lengo, walifikiwa. • Pamoja na kuelezwa madhara ya kukaa pembeni kama 'watazamaji' badala ya kushiriki kuzuia rushwa, walielimishwa kwamba miradi ya maendeleo ni mali

		yao na hivyo wana wajibu wa kuisimamia • Tunaendelea kuwahimiza walioelimishwa, wawe mabalozi wetu kwa kupeleka elimu waliyopata kwa wananchi wengine na zaidi wawe chachu ya mabadiliko kivitendo kwamba kuzuia rushwa ni jukumu la kila mwana Dodoma na si kazi ya Serikali pekee.
3.	Kutembelea na kuziimarisha Klabu za Wapinga Rushwa katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo.	Klabu za Wapinga Rushwa zimetembelewa mara 89. - Kumekuwa na mwamko mkubwa wa vijana katika kupinga rushwa na kukuza maadili ya kitanzania ya kuzingatia haki na usawa.
4.	Semina ya kuhamasisha nafasi ya walimu walezi wa klabu katika shule za msingi na sekondari jijini Dodoma	Kupitia Semina hii, mikakati ya kuziimarisha Klabu za Wapinga Rushwa iliwekwa.
5.	Kuendesha Semina 27 makambini na mashuleni, kwa kushirikiana na Chama cha Skauti chini ya mpango wa TAKUSKA.	Mafunzo ya kukuza uzalendo, uwajibikaji na uadilifu kama nyenzo muhimu ya kujenga kizazi kinachochukia rushwa, yalitolewa.
6.	Kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2022	Wito wa 'Vunja Ukimya: Kataa Rushwa ya Ngono' ulitolewa
7.	Kuelimisha washiriki kwenye maadhimisho ya WIKI YA SHERIA	Elimu kuhusu umuhimu na wajibu wa wananchi kushiriki kuzuia rushwa ilitolewa.

Vilevile, elimu dhidi ya rushwa ilitolewa kupitia Semina 50, Maonesho 5, Vipindi vya redio 18 na kipindi kimoja cha televisheni.

Pili, katika eneo la **UZUIAJI RUSHWA** na kwa kuzingatia kwamba miradi ya maendeleo ni mali ya wananchi na Serikali inapeleka fedha nyingi katika eneo hilo, TAKUKURU Mkoa wa Dodoma **imefuatilia utekelezaji wa miradi arobaini na moja (41)** yenye thamani ya **shilingi bilioni 11.2** (11,221,281,331/=) katika sekta za Ujenzi, Elimu, Afya na Maji. Hii inajumuisha miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19.

- Miradi 10 (sawa na asilimia 24), ilikuwa na mapungufu madogo kama ya kuchelewa kukamilishwa kwa mujibu wa mkataba, jambo linalosababisha kuongezeka kwa gharama; vifaa visivyokidhi ubora; pamoja na manunuzi kwa gharama zaidi ya bei ya soko.
- Mapungufu husika yalirekebishwa kwa kutoa elimu na kusimamia marekebisho kwa kushirikiana na wadau.
- Mradi mmoja ulionekana kuwa na viashiria vya jinai na hivyo uchunguzi umeanzishwa.
- Aidha, shilingi 409,454,543/= zilizolipwa kwa wakandarasi kinyume na taratibu katika utekelezaji mradi mmoja zilirejeshwa kwa kushirikiana na halmashauri husika.

Pale ambapo eneo la utendaji au utoaji huduma linaonekana au kulalamikiwa kuwa na viashiria vya rushwa, TAKUKURU hufanya **uchambuzi wa mfumo** ili kubaini iwapo kuna mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuiziba.

- Tumefanya **chambuzi sita** za mifumo katika sekta za mapato, elimu na ujenzi.
- Tumebaini kwamba, pamoja na mambo mengine, kuna utitiri wa leseni za uchimbaji wa madini na ujenzi lakini maeneo mengi hakuna kinachoendelea na hivyo kuzinyima halmashauri mapato. Mfano wilayani Mpwapwa kuna leseni za wachimbaji 773 lakini zinazotumika ni 57 tu.
- Pia halmashauri zinapoteza mapato katika maeneo ambayo uchimbaji unafanyika kiholela na ambayo hayana mashine za POS.
- Kwenye uchambuzi wa mfumo wa viashiria vya rushwa ya ngono katika sekta ya elimu ngazi ya halmashauri, imebainika kuwa maeneo hatarishi kwa uwepo wa rushwa ya ngono ni upangaji wa vituo vya kazi kwa asilimia 72 na uhamisho ndani ya halmashauri kwa asilimia 63.
- Kwenye uchambuzi wa mfumo wa ujenzi wa Shule Shikizi, imebainika kuna ufahamu mdogo kwa Kamati za Shule kuhusu matumizi ya mfumo wa manunuzi wa 'force account'.

- **Warsha tano** za kujadili matokeo ya uchambuzi wa mifumo kwa kushirikisha wadau zilifanyika katika sekta za elimu na ujenzi ambapo maazimio ya namna ya kuziba mianya ya rushwa yalifikiwa na muda wa utekelezaji kuwekwa. Vilevile, taarifa mbili za utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa siku za nyuma katika sekta za ardhi na afya zilipokelewa.

- Tunawakumbusha wote wenye wajibu wa kufanyia kazi maazimio ya kuziba mianya ya rushwa bainishwa, kutekeleza wajibu wao kwa wakati.

Tatu; Pamoja na kuhamasisha sana suala la **KUZUIA RUSHWA,** bado wapo ambao ni 'sikio la kufa ambalo halisikii dawa'. Hivyo tumepokea **malalamiko 113,** ambapo taarifa za rushwa zilikuwa 66 na zisizo za rushwa ni 67. Hizi ni nusu ya taarifa zilizopokelewa katika robo kama hii mwaka 2021 jambo ambalo linaashiria kwamba kampeni ya uzuiaji rushwa inaonyesha mafanikio.

- Taarifa zinazohusu rushwa zilihusu sekta au maeneo yafuatayo: Serikali za mitaa (19); Elimu (10); Afya (9); Polisi (5); Mahakama, Ardhi na Sekta binafsi (kila moja 4) na sekta nyinginezo (11).
- Taarifa 66 zinazohusu rushwa zimeshughulikiwa kwa mujibu wa sheria kwa njia za uelimishaji, uzuiaji pamoja na uchunguzi.
- Majalada 16 ya uchunguzi yamekamilika na mashauri 8 mapya yamefunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya mashauri yanayoendelea mahakamani kufikia 58. Idadi ya mashauri yaliyoamuliwa katika kipindi hiki ni matatu ambapo Jamhuri ilishinda katika shauri moja.
- Kati ya taarifa 67 zisizohusu rushwa, 2 zilihamishiwa idara zingine na wahusika wa taarifa 65 zilizosalia walishauriwa mahali sahihi pa kuziwasilisha na wengine walipelekwa taasisi stahiki kwa msaada na hivyo taarifa hizo zikafungwa. Nusu ya taarifa zisizohusu rushwa zilihusu sekta za ardhi na binafsi.
- Tunaendelea kuwasihi wananchi kufuatilia elimu tunazotoa ili watuletee tu malalamiko yanayoangukia kwenye Sheria ya Kuzuia na Kupambana na rushwa Sura ya 329 kwani bado wengi wanawasilisha kwetu masuala ya taasisi zingine.

Nne, MIKAKATI YA APRILI – JUNI 2022:

TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, inatarajia katika robo ya Aprili-Juni, 2022 kuimarisha juhudi za kuzuia rushwa kwa kukagua miradi ya maendeleo na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika vita dhidi ya rushwa kupitia nyenzo mbalimbali za uelimishaji ikiwemo mkakati wa TAKUSKA, vipindi vya redio pamoja na uelimishaji katika mikusanyiko mbalimbali.

Pia tutaendelea kufuatilia makusanyo na uwasilishaji wa mapato yanayotokana na mashine za POS na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za umma.

Aidha, tutafanya warsha na wadau kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo zilizokamilika ili kuweka maazimio ya namna bora ya kuziba mianya ya ufujaji iliyobainishwa.

Pia tumejipanga kufanya kongamano kwa walimu walezi wote wa mkoa mzima katika robo ya Aprili-Juni, 2022.

Mwisho, tunawashukuru wananchi wa mkoa wa Dodoma kwa kutuunga mkono katika vita hii yetu sote. Tunawasihi wengine wote wenye mtazamo kwamba hii ni kazi ya Serikali pekee waachane na fikra hizo batili na wajiunge kuongeza nguvu katika jeshi la wazalendo, waadilifu na wanaojisikia fahari kuzuia rushwa. Umoja ni nguvu. **RUSHWA HAILIPI**.

Imetolewa na:

Sosthenes W. Kibwengo
Mkuu wa TAKUKURU (M) Dodoma
Simu: 0738150070